SEBHA UNIVERSITY JOURNAL OF HUMAN SCIENCES VOL.21 NO. 1 2022
DOI: 10.51984/JOHS.V21I1.1397

مجلة جامعة سبها للعلوم الإنسانية
Sebha University Journal of Human Sciences

Journal homepage: https://sebhau.edu.ly/journal/index.php/johs

# Tofauti Na Kufanana Ya Ada Za Harusi Baina Ya Waswahili Na Walibya

Salem Mahmoud Abdulhadi Massoud

African Languages, Faculty of Arts, Sebha University, Libya

**Keywords:**
Harusi
Ada
Walibya
Kufanaan
Historia.

**A B S T R A C T**

Makala hii ilikusudia kuchunguza tofauti na kufanana baina ya harusi ya Waswahili na Walibya. Madhumuni yalikuwa Kubainisha tofauti za ada za harusi baina ya Waswahili na Walibya. Lengo hasa ni kuona kiasi gani ya ada hizi hutofautiana na kufanana. Makala hii ilfanywa Zanzibar na Libya. Data zilipatikana kutoka kwa wanaofahamu ada hizi. Hawa walikwa ni wanawake na wanaume wazee wanaofahamu ada za harusi na taratibu zake kutoka sehemu zote mbili. Pia watafiti walishuhudia ada hizo katika harusi. Aidha, taarifa nyingine zinapatikana katika vitabu kuhusu historia na utamaduni wa Waswahili wa Zanzibar. Hata hivyo Makala itakuwa na umuhimu kwa wanafunzi wa somo la utamaduni kujua ada za harusi za Waswahili na Walibya. Vile vile wageni watokao nje ya Zanzibari wanaotaka kujua utamaduni wa jamii ya Wazanzibari au hata ya Walibya wataweza kufaidika na Makala hii

## الأختلاف والتشابه بين السواحليين والليبيين

سالم محمود عبدالهادي مسعود

قسم اللغات والدراسات الإفريقية، كلية الأداب، جامعة سبها، ليبيا

**الكلمات المفتاحية:**
العروس
العادة
الليبيين
التشابه
التاريخ

**الملخص**

تهدف هذه المقالة إلى استكشاف أوجه الاختلاف والتشابه بين حفلات الزفاف السواحيلية والليبية. كان الهدف هو تسليط الضوء على الفروق في رسوم الزفاف بين السواحيلية والليبيين. الهدف الرئيسي هو معرفة مقدار هذه الرسوم التي ستختلف وتتناسب. تم الحصول على البيانات من أولئك المطلعين على هذه الرسوم. كان هؤلاء من النساء والرجال المسنين الذين يعرفون رسوم وإجراءات الزفاف من كلا المكانين. كما شهد الباحثون الرسوم في حفل الزفاف. بالإضافة إلى ذلك ، تتوفر معلومات أخرى في كتب عن تاريخ وثقافة الشعب السواحلي في زنجبار. ومع ذلك ، سيكون المقال مفيدًا لطلاب الدراسات الثقافية لمعرفة رسوم زفاف السواحيلية والليبيين. وبالمثل ، سيتمكن الزوار من خارج زنجبار الذين يرغبون في معرفة ثقافة الزنجبار أو حتى الجالية الليبية من الاستفادة من هذه المقالة.

## UTANGULIZI

Kwa kawaida katika jamii zote ulimwenguni neno harusi si kitu kigeni miongoni mwao. Na kila jamii zina mifumo yake ya harusi ambayo huyatumia wakati wa jambo hilo linapofika. Ama kwa ujumla harusi ni ile hali ya mwanamme na mwanamke aghlabu waliolauisha kuwa baleghe kuwekwa pamoja kwa mujibu wa sharia na kanuni waliozokubalia.

Na ili kuhalalisha maingiliano ya kimwili. Takriban jamii nyingi ulimwenguni hufanya hivi ingawa ndani yake hujitokeza tofauti kadha wa kadha katika ada zao za harusi.

Hilo ni jambo baya yapasa tulipige vita jamii zote za kibinadamu kwa ujumla. Kwani katika jamii zetu tumeshuhudia kuona harusi za mataifa mbali mbali ulimwenguni zikiwa na ada zao kamili. Nasi tukiziona tu hujuwa kama kitendo kile sasa ni sehemu moja wapo ya harusi.

Baada ya kuona hayo, watu wengi hupelekea kuzisifu au

*Corresponding author:
E-mail addresses: sal.massoud@sebhau.edu.ly

*Article History : Received 15 August 2021 - Received in revised form 29 March 2022 - Accepted 15 May 2022*

kuzipenda kwa kuzifananisha na kuzilinganisha ada hizo zikiwa zimewapendeza au laa!

Hata hivyo, mara nyingi tumekuwa tukipendezwa na vipengele hasa vile ambavyo vina muonesha harusi wa kike na bwana harusi wakiwa wamevalia mavazi yao rasmi ya kutoka mbele za watu. Jinsi walivyopendeza kwa mapambo yao mbali mbali.

Pamoja na taratibu za mikao ya mahala pa harusi na utulivu wenye kupendeza. Hali hii huwafanya watu wa jamii mbalimbali kuiga baadhi ya mambo na kuyaingiza katika mila za desturi zao za harusi kwa ujumla.

Ingawa kwa ujumla wake, mila au ada hizi za harusi zimegawika katika sehemu mbili kuu. Miongoni jamii nyingi ulimwenguni yaani za asili na zile za kigeni.

Kwa kufupisha utangulizi wa ada harusi tunadirika kusema kwamba, watu wanapaswa kufuata ada za harusi katika misingi inayokubalika kisheria na Kanuni ambazo mtu yoyote akiiyona ada hiyo ya harusi asishangae sana. Kwa sababu, kuna mambo mengine hata kama si ya mila yako au ada yako basi huweza kuyapenda na kufurahika. Vile vile yako mengine hukuhuzunisha tu, kwa kuchupa mipaka ya kiutu na ubinadamu.

### 1.1. Madhumuni ya Makala:

Madhumuni ya Makala huu yaliukuwa yafuatayo:

(1) kubainisha au tofauti na kufanana baina ya harusi za Waswahili na Walibya.
(2) Kubainisha tofauti na kufanana baina ya ada za harusi za Waswahili na Walibya.

### 1.2. Maswali ya Makala:

Makala huu uliongozwsa na maswali yafuatayo:

(1) Je, kuna tofauti na kufanana baina ya harusi za Waswahili na Waliby?
(2) Ni ada gani ambazo ni tofauti na kufanana baina ya harusi za Waswahili na Waliby?

### 1.3.Umuhimu wa Makala:

Makala huu unatarajiwa kuwa na umuhimu ufuatao.

(1) Kujua ada za harusi za Waswahili na Walibya.
(2) Kufahamu kuhusu utamaduni wa Waswahili na Walibya katika harusi zao.
(3) Makala itatumika kama marejeo maktabani.
(4) Makala utatoa mwongozo kwa watafiti wengine kuendelea kufanya tafiti zaidi kama vile kujua utamaduni na ada nyengine kwa Waswahili na Walibya. Au hata kuendeleza zaidi makala huu katika ngazi ya juu kama vile: uzamili na uzamifu.
(1) Aidha, wanafunzi wasomo la utamaduni watweza kufaidika zaidi kufahamu tamaduni za harusi za Waswahili na Walibya.

### 1.4. Ukusanyaji wa Makala:

Data zilipatikana kutoka kwa wanaofahamu ada hizi. Hawa walikwa ni wanawake na wanaume wazee wanaofahamu ada za harusi na taratibu zake kutoka sehemu zote mbili. Pia watafiti walishuhudia ada hizo katika harusi. Aidha, taarifa nyingine zinapatikana katika vitabu kuhusu historia na utamaduni wa Waswahili wa Zanzibar.

### 1.5 Maelezo ya Istilahi

*Ada:* Ni jambo la kawaida ambalo hufanywa kila siku au desturi ya watu.

*Hufana:* Namna ya jambo linavyofanyika kama lilivyokusudiwa vizuri sana.

*Fungate:* Ni siku maalumu za ufanyikaji jambo kama vile harusi, kwa mfano 3, au siku saba au saba moja.

*Tazuo:* Kitu cha thamani anachopewa biharusi na mumewe baada ya kukutika na mtoto (bikira).

*Jaliko:* Ni kitendo cha wanawake wa zamani kwenda kikundi kualika harusi kila kikundi kualika harusi kila kijumba au nyumba.

*Mshenga:* Ni mtu anayekwenda kupeleka posa kwa mtoto wa kike.

*Mbanjo:* Nguo anazonunua mume na familia yake kwa ajili ya mke wake.

*Matandiko*: Ni magodoro yanayotandikwa kitandani kama la usufi au sponji.

*Makungwi*: Ni mwanamke au wanawake wanaokaa na maharusi na kuwafandisha namna ya kuishi katika ndoa.

*Singo*: Miongoni mwa mambo ya usafi wanaoyofanyiwa maharusi ya kusafishwa kwa kusuguliwa mwili kwa viungo vya maua makavu ya unga. Kama vile unga wa karafu, liwa, dalia na sandali.

*Tumbuizo:* Nyimbo zinazoimbwa kwa mahadhi fulani katika harusi au sherehe yeyote ile.

*Turu*: Ni kitu au chakula kawaida kisicho cha kila siku.

## HARUSI ZA WASWAHILI, ZANZIBAR

### 2.1 Utangulizi

Sura hii inazungumzia zaidi taratibu na ada mbalimbali zinazofanywa katika harusi za Waswahili Zanzibar. Aidha, tumeeleza pia ada za asili na za kutoka njia zilizoingia katika harusi za Waswahili.

### 2.2 Ada na Sherehe za Harusi za Wazanzibar

Harusi za Waswahili wa wana desturi na mila zao katika kusherehekea harusi zao. Jamii hii ina utamaduni au ada inchanganyiko wakati wa kusherehekea harusi. Upo utamaduni wa Kiafrika na utamaduni wa Kiarabu/Kiisilamu. Katika harusi zao ngoma na nyimbo zao zimekuwa katika hali ya mchanganyiko wa Ubantu na Uarabu.

Ada harusi za Zanzibar tunazoshughulikia zinajumuisha visiwa vyote viwili yaani Unguja na Pemba. Pamoja na hava kuna mambo kwa ujumla ambayo hufanyika kwa wakati wa harusi.

#### 2.2.1. Posa na kutafuta Mchumba

Mara nyingi sana kidesturi, kiutamaduni na kidini watu wa Zanzibar katika familia zao wakishaona kama mtoto wao wa kiume ameshitimia umri wa baleghe. Huwaita watotwo wao wa kiume na kuwashauri kuhusu suala la kuoa. Kwa familia nyengine zikona zina watoto wakike ndani wamekaa tu hawasomi au hawana jambo la msingi la kuwaziwa wasiolewa. Basi liwenda katika familia fulani na kushauriana wawaoze watoto zao iliwaunge udugu zaidi.

Haya hufanyika mara nyingi kwani familia za hapa Zanzibar. Asili na asili hawapendi watoto wao kuwaona wanatumbukia katika janga la uchafu wa zinaa. Hivyo basi hufanya hivi ili kuwanusuru watoto wa kike au familia isije ikawa na watoto wanje ya ndoa.

Aghlabu mchumba anaweza kupatikana kwa kupitia mtoto wa kiume mwenyewe kusema (mimi) nnae mchumba yuko sehemu fulani au kusema mie sina inchumba mnitafutie. Pia wakati mwengine, watoto wa kike na wakiume kukutana wenyewe na kupeana shauri kwamba mvulana apeleke wazazi wake kwa msichana ili wakapose. Nia zote hizi zinatokea siku hizi.

Hapo tena hufanywa hivyo na aghlabu wazazi wa mvulana ndio wanaokwenda kwa msichana kuposa hata kama wazazi wa msichana ndio waliotoa wazo hilo.

Kwa kawaida katika posa za Kizanzibar wanapokwenda kupeleka posa hufanyayafuatayo. Kwanza hutafuta mtu

maalumu mwenye heshima anaetambulikana katika familia ile anayeitwa. Mshenga hwenda katika famalia ya msichana na kutoa neno la awali au kudokeza na familia ya msichana. Iwapo wataafikiana nalo
humpa jibu kwamba wende wakapeleke posa rasmi. Hii inaweza kuwa siku ile au nyengine. Huambiwa au kukatwa (mahari) wengine hutoa pale pale. Na wengine upanga siku maalumu ya mahari kwa mkewe mtarajiwa na ndio hapa ushirika wa mwanzoni wa wanawake wa msichana kwenda kukagu nyumba atakayokaa, mwana wao na kuitafutia mapambo kama mapazia na kadhalika.

**2.2.2. Mahari:**

Baada ya kukubaliwa posa hufuata mahari. Waswahili hutoa mahari kwa kufuata mafundisho ya dini ya Kiisilamu. Mahari yanategemea uwezo wa mtu hakuna kina maaluumu. Mahari va Waswahili aghlabu huwa kama vile:

(i) Fedha Vitu vya samani mfano:- kitanda, kabati na makochi.
(ii) Vyombo vya dhahabu mfano:- mkufu, bangili, pete na hereni.
(iii) Wazee wa maharusi hupatana na kusikilizana siku ya kuleta mahari. Mahari laitolewi kwa siri, aghlabu hupeleka kwa sherehe na nyimbo.

Siku ya kupokea mahari watu wa upande wa mke huwakaribisha watu wa mume kwa heshima. Baada ya kukaa, mzee katika watu wa mume hutoa mahari kumpa mzee katika watu wa mke. Mahari huhesabiwa mbele ya watu, na tena hupelekwa ndani kwa wanawake kuhesabiwa tena. Wanaume huandaliwa vyakula na kupigwa " Sherha -ha" na kwenda zao. Wanawake pia wanaandaliwa vyakula.

Baada ya mahari kutolewa, hushauriana juu ya siku ya harusi. Baadhi yao, kabla ya kutolewa siku ya harusi, wazee wa mke na wa mume huenda kwa waganga kutafuta *manuzili.* (Yaani saa mwafaka ya kufunga ndoa).

Wanawake wa upande wa mume wanapokuwa njiani kupeleka mahari kwa watu wa upande wa mke aghlabu huimba nyimbo hizi:

*JAHAZI*
*Jahazi yetu twaipeleka kwa pepo njema.*
*Nenda mwanangu amana Llahu Aman*
*Rasuli. Huyo ajoye mwana wa siwa na matuwozi*

**2.2.3. Kualika Harusi**

Baada ya kukubaliana juu ya siku ya harusi. kinachofuatia ni ualikaji. Zamani ualikaji wa kusherehekea harusi ulikuwa kwa siku nyingi: lakini siku hizi sherehe huwa siku mbili hadi tatu. Waswahili husherehekea harusi mwaka mzima isipokuwa mfungo nane/Safar. (Safar ni mwezi wa pili Kiisilamu). Waswahili wanaitikadi huu ni mwezi wa kisirani au nuhusi kwa mtu kufanya harusi.

Harusi za Waswahili hualika kwa njia zifuatazo:

(i) Kwa njia ya kadi
(ii) Kunadi katika msikiti au maklabu
(iii) Kundi la wanawake (majaliko) kwenda kualika katika kila nyumba
Wana ozitaka.

Kwa mfano Kuna wale wanaoalika kwa kadi. Kadi hivo hutiwa:

- ✓ Jina la wazee wa mume.
- ✓ Tarehe na saa ya nikaha
- ✓ Pahala nikaha itakapofungwa.
- ✓ Hutaja siku ya walima
- ✓ Hutaja ukumbi ambao bibi harusi atapambwa

**2.2.4 Singo:**

Singo ni moja kati ya ada anazofanyiwa bwana au bibi harusi mtarajiwa wa Kizanzibari. Ada hii hufanywa siku chache kabla ya kufunga nikaha. Wanaohusika na kusinga ni kungwi na watani wa harusi. Watani hawa wanaweza kuwa bibi, binamu, wifi au mashoga marafiki).

Singo, kwa mujibu wa muhojiwa mmoja alivehojiwa anaeleza, ina lengo la kumtoa bibi harusi katika hatua ya utoto na kumuingiza katika hatua ya utu uzima. Mbali na hayo, kwa mujibu wa wasingaji wa kileo wanasema kwamba singo ina lengo zaidi hilo. Kwa mujibu wao wanadai kwamba lengo jingine la singo ni kumuweka bibi harusi tayari kukutana na mwenzi kimwili.

Kabla ya nikaha. kungwi mkuu humuusia mwari kuhusu shughuli atakayofanyiwa siku hiyo. Huambia kwamba mambo atakayofanyiwa asivaeleze nje kwa mashoga zake kwani ni siri ya ndani. Vile vile ayazingatie yote atakayofundishwa kwani ni muhimu katika maisha yake ya ndoa

Mwari huanza kusingwa kwa vifaa ambavyo tayari vimekwishatayarishwa. Kusinga huko huanzia usoni. Uso husingwa kwa rojo la liwa lililochanganywa na maua yenye kutoa harufu nzuri yaliyokaushwa na kusagwa. Mfano wa maua hayo ni asumini, vilua manjano na mawardi. Pia, mchanganyiko huo hunyunyiziwa mafuta mazuri kama ya *al wud.* Ama kwa upande wa mwilini. usingaji hufanyika kwa rojo kilma la usoni lakini hilo huongezwa unga wa karafuu.

Mwari hasingwi kimya kimya. Nyimbo huimbwa huku tendo la kusinga ikiendelea. Kwa upande wa niwari wa kiume wanaoimba huwa wako nje ya chumba cha kusingia. Lakini kwa mwari wa kike wanaosinga huimba pia. Nyimbo mbali mbali huimbwa wakati huu.

Wakati wa kusingwa huimbwa nyimbo na watu kucheza. Nyimbo za singo huwa zinaeleza mafundisho. Mfano wa nyimbo za singo:

KUNA ILA MOJA

| | |
|---|---|
| Kungwi: | Kuna ila moja ila, ila mama ila,<br>Uchafu uache ilo. |
| Kungwi: | Kuna ila moja ila, ila mama ila,<br>Kuwapuuza wokwe ila. |
| Kungwi: | Kuna ila moja ilo, ila mama ila,<br>Kidogo nda kwetu ila. |
| Kungwi: | Kuna ila moja ila, ila mama ila,<br>Kila siku kwa mama ila. |
| Kungwi: | Kuna ila moja ilo, ila mama ila,<br>Kusimbulia chakula ila. |
| Kungwi: | Kuna ila moja ila, ila mama ila,<br>Siwezi kupika ila. . |
| Kungwi: | Kuna ila moja ila, ila mama ila,<br>Ujuba uuache ila. |
| Kungwi: | Kuna ila moja ila, ila mama ila,<br>Nyumbani kufagia ila. |
| Kungwi: | Kuna ila moja ila, ila mama ila,<br>Leo nimechoka ila. |

**2.2.5. Kufunga Nikaha/Akdi**

Nikaha hufungwa msikitini au nyumbani kwa wazazi wa bibi harusi. Waswahili ufunga nikaha zao kufuata sheria ya dini ya Kiisilamu. Kabla kadhi hajafungishia nikaha husomwa Kuruan tukufu, kisha hutolewa khutba ya nikaha kwa mukhtasari. Aghlabu kadhi kwa niaba ya wakil (baba bibi harusi) hufungisha nikaha. Kadhi humshika mkono bwana harusi na kumwambia asema maneno fulani atakayo sema: Maneno hayo ni "fulani bin fulani umekubali kumuoa fulani binti fulani kwa mahari muliyo Kubaliyana" Bwana harusi akishakubali kadhi naye husema "Nami nimekuwaozesheni kama alivyoamrisha Mwenyezi Mungu". Baada yahapo hutiwa *fatiha* na duwa ya kuwaombea maharusi. Aghlabu hutolewa haluwa na kahawa chungu.

**2.2.6 Kutoa Mkono:**

Baada ya nikaha kufungwa bwana harusi lazima ende nyumbani kwa bibi harusi na kumpa mkono. Kisha humchukua mkewe na kwenda naye kwake. Au wakati

mwengine baada ya kutoa mkono humuacha na kurudi baadaye usiku kumchukua. Baada ya kutoa mkono. kula na mambo mengine kama kupiga picha waume humchukua mke wao.

**2.2.7 Walima**

Hiki ni chakula maarufiu ambacho huandaliwa baada ya siku moja kufungwa nikaha. watu wengine walima huandaliwa siku ileile ya nikaha iwapo nikaha itafungwa baada ya mshuko wa sala ya adhuhuri. Aghlabu kwa harusi nyingi za Waswahili walima huwa ni wali wa briani na vinywaji kama juisi au soda.

**2.2.8 Kuchukua Mke:**

Waume wanapokwenda kuchukua mke huimba. Wakifika ndugu wa bibi harusi huwakaribishwa na kuwatafutia mahali pa kukaa. Wakisha kukaa ndugu wa harusi humuita mame harusi aje awaone wageni.

**2.2.9 Harusi kujibu:**

Siku ya pili ya ndoa, aghlabu kungwi huenda kuangalia kama ndoa imejibu au la. (kuangalia kama bibi harusi alikuwa bikra). Majibu yakipatikana watu huimba wakizunguka mitaani.

Bibi harusi akipatikana ni bikira bwana harusi hutoa zawadi/hidaya kwa bibi harusi. Watu huimba na kumpa hongera bibi harusi pamoja na mamake bibi harusi.

**2.2.10 kukabidhi Sanduku:**

Bibi harusi hupewa sanduku kutoka kwa mume Sanduku hili huwa lina vitu vya bibi harusi kama vile nguo, viatu, uturi, podari, shanga n.k. Aghlabu bibi harusi hukabidhiwa sanduku siku ya pili baada ya walima (karamu ya chakula cha mchana).

**2.1.11 kuwatoa Maharusi:**

Siku hii maharusi hupambwa na kutolewa kweye ukumbi. Baadhi husherekea kwa kupiga taarab. Wengine husherekea kwa kusoma *Maulidi* ya Mtume Mohammad (s.a.w). Kasida hizi huimbwa pamoja na kupiga madufu.

Bibi harusi hukalishwa kwenye kochi zuri akipigwa picha na watu wakiimba, Marafiki huchukua fursa hii kumpa zawadi bibi harusi. Baada ya kuimba, hutolewa dhifa watu kula.

Mtu mmoja kwa niaba ya famila ya bibi harusi husimama na kutoa shukrani na kuwatakia kheri wageni wote waliohdhutia . Baada ya hapo kila mtu anaenda kwake. Aghlabu hii ndiyo shughuli ya mwisho katika harusi. Baadaye bwana harusi humchukuwa mke wake na kwenda kuanza maisha yao mapya.

**2.3 Ada za Asili na kigeni katika Harusi za Wazanzibar**:

Mambo haya nayo kama kawaida yamegawika katika sehemu mbili nazo ni ada za asili kabla ya ujio wa wageni na zile ada zilizopatikana baada ya maingiliano ya Waswahili. Ada hizo zimeonyeshwa hapa chini.

**2.3.1 Ada za Asili ya Unguja**

Hizi ni ada za asili za Unguja kabla watu wa nnje hawajafanya makazi yao Zanzibar, Ada hizi ni pamoja na:

(a) Mkutano
(b) Kushindika tambi (mito na matandiko-magoro)
(c) Kutia pamba
(d) kutona kipaji
(e) Kuwasinga maharusi.
(f) Kukosha maji ya ndoa
(g) Kuvaa visutu
(h) Kupeleka vyombo hasa nguo kutoka kwa mume
(i) Kuwangoja maharusi

Aidha, mbali na hizi ada tulizozitaja hapa juu pia kuna ada za asili ya harusi ya Mswahili wa Kizanzibari kama vile: kukosha maji ndoa, kuvaa visutu, kupeleka vyombo na nguo kutoka kwa mume (sanduku) na kuwa wa ngoja maharusi yaani kuamgalia kama harusi imejibu au la. Hizi ni ada utazikuta katika harusi za Ungujit na Pemba. Zilikuwa zikifanywa na kufanywa kabla ya watu wa nje hawajafanya makaazi yao hapa visiwani.

**2.3.2 Ada za kigeni katika Harusi za Wazanzibar**

**2.3.2.1 Ada za Waarabu wa Hadhramout**

(i) Kukamata.
(ii) Kumkosha nywele bi harusi kwa damu ya mbuzi.
(iii) Kumtia hina bwana harusi kwa sherehe.
(iv) Kutwanga buni.
(v) Kumchezesha bi harusi.
(vi) Bi harusi kuvaa kanzu ya kijani siku ya kutia nyumbani.
(vii) Bwana harusi kutompa mgongo mkewe.
(viii) Kuamkia wazee wa mke.

Bwana harusi kufungo cha rohoni cha fulana alu kanzu kama bibi harusi akiwa mtoto mdogo

**2.3.2.2 Ada za Waarbu wa Omani:**

(i) Bwana harusi kufungo cha rohoni cha fulana au kanzi kama bibi harusi akiwa mtoto mdogo.

**2.3.2.3 .Ada ya Waarabu ya Waajemi**:

(i) Kuwakosha miguu maharusi.

**2.3.2.4 . Ada za Kizungu**

(i) Bwana harusi kumpeleka pete ya uchumba.
(ii) Kumvalisha veli bi harusi na kumuweka pamoja na watoto yaani *"bridemaids"*.
(iii) Kuvaa suti
(iv) Kupiga picha
(v) Bwana harusi na bibi harusi kukaa pamoja mbele za watu na watu kuchukuana mikono kwa mkono
(vi) Kwenda "*one-moon*"

**2.3.2.5. Ada za Kisilamu**

(vii) Walima
(i) Kumsomea bi harusi juu ya kichwa
(ii) Kusali na kuomba kheri siku ya kwanza bwana na bibi kabla kukutana kimwili.
(iii) Kuloa jazua.

Kwa mujibu wa haya itazidi kudirika ya kuwa ada za harusi za Kiunguja ni mchanganyiko wa ada za harusi za makabila yote yaliyofanya masakani yao hapa au yaliyoleta usataarabu wao huku. Wakaazi wanafuata ada za asili za kikwao, na ada za asili za kiunguja na baadhi za Kizungu katika maharusi.

Kwa ujumla hizi ndizo ada ambazo zinafanywa na wakaazi wa Zanzibar wa makabila tafauti. Kama tulivyosema hapo awali. kwamba. Zanzibar ni Ungaja na Pemba na wa hivi vinakliwa na watu wenye makabila lafauti ambao wote hufanya harusi za kufuata baadhi ya vipengele. Aidha, ni vigumu kufuta mambo yote hayo kwani kila mtu au kila jamii huzingatia au huchagua lile analoliona ni muhimu kwao kwa mujibu wa hadhi zao na pesa zao au uwezo wao.

**HARUSI ZA WAARABU, LIBYA.**

**3.1 Utangulizi**

Kwa kawaida harusi Libya huanza hasa pale shule au skuli zinzpofungwa ambapo watu wote huwa wapo nyumbani wakati wa likizo na aghlabu huwa ni kama mwezi wa tisa.

Ada za harusi katika Libya huenda pamoja na siku za wiki ya kuanzia Jumatatu mpaka Ijumaa, au wengine mpaka Jumamosi na Jumapili.

Pia Libya kwa vile hakuna wageni wengi ambao

wamechanganyika pamoja tumeou kwamba, mambo yao hayajabadilika sana kwa kufuata mila tofauti tofauti na zile za asili yao.

Ingawa kang makabila meyine nchini Libya lazima wakumbane na wimbi la mabadiliko ya kijamii kiutamaduni. Wamejikuta wakikumbana nayo mambo hayo bila ya kutarajia kwa mnila au ada za harusi nchini Libya. Hivyo wimbi hili kwa kiasi fulani imethiri ada za harusi hasa zile ada zinazofanywa na katika harusi a Kizungu. Ufafanuzi zaidi wa ada za hizo tutazieleza baadve. Hata hivyo, miongoni mwa ada za Walibva ni hizi zifuatazo:

**3.2 Ada na Sherehe za Harusi za Waliby:**

**3.2.1. Posa na kutafuta Mchumba**

Familia ya mvulana baada ya kumuona mtoto wao sasa ameshafukia umri wa kuoa au ana uweza wa kumudu ndoa ni kumuuliza na kumshauri kutafuta mchumba kama anae husema na kama hana wazazi wake hujifunga kebwebwe kumtafutia.

Na bwana harusi nae hujipanga kutafuta na kukusanya pesa. Katika utamaduni wat Walibva ni kuwa, majukumu mengi ya harusi hufanywa na familia ya mvulana.

Baadaye mama na dada mkubwa wa bwana harusi huingia kutafuta msichana. Baada ya kuuliza historia ya msichana na familia ya mvulana na wao pia hufanya hivyo. Uchumba ukisha kamilika na kupatikana binti kila wapnde wa familia hukulana mwanzo kivyao. Baadaye familia mbili za bwana na bibi) hukutana na kuanza kupanga mambo mbalimbali na kuandaa shughuli kamili ya harusi.

**3.2.2 Mahari**

Familia ya msichana kukaa pamoja na kukata mahari. I lapo tena kwa hatua za awali bwana harusi na familia yake wao ndio hasa wafanyaji shughuli Mahari ya Walitiva huwa ni dhahabu na pesa taslim. Mbali na mahari mume anayetaka kuoa lazima apelike *"halib mama"* (mkaja au maziwa ya mama) aglabu huwa kitu kidogo lakini wengine huambiwa watoe bagili za dhahabu. Pia mume atakiwa apelike ngamia kama ada atakayetumika katika siku za harusi kwa upande wa bibi harusi. Zaidi ya yote mume anayetaka kuoa lazima awe amrjrnga nyumba. Ni wa chache wanaopanga au kukodi nyumba kuanza maisha yao. Vile vile mume anaveoa inapendezeka awe na kipando hasa gari.

**3.2.3 Matayarisho ya Harusi**:

Katika harusi za Walibya matayarisho au maandalizi huwa kabla ya harusi na wakali wa harusi na baada va harusi. Walibva hujiandi hwa harusi kwani baada ya kun tulivyoona baada ya koo mbili kukutana.

Kwa walio wengi harusi za Walibva huanza siku ya Jumanne. Hii ni siku ya bwana harusi na familia vake kupeleka *waliima. A*idha, siku hii pia ni siku ya *wallijau y*aani kupeleka nguo ya bi harusi na mavazi pamoja na chakula. Siku huwa na mwaliko wa familia ya bwana harusi kuwaalika jirani zake kula chakula pamoja. Bandaye bwana harusi na familia yake watachukua nguo za bibi harusi au mavazi ya bibi harusi pamoja na chakula kama alizeti debe moja mchele. sukari. mboga mboga kama tungule, mabilinga, unga wa ngano, sabuni, kondoo mkubwa u mbuzi au ngamia IN kupeleka kwa bibi harusi.

Vilevile siku watu hualikwa kwa bwana liarusi kula chakula cha na mchana na jioni na kupata mwaliko huu watu kutoka sehemu mbali mbali uja na kusherekea panojil na kucheza, kuuimba na kupiga vigelegele.

Siku ya Jumatano, ni siku ya ukoo wa bwana harusi kupeleka mavazi kwa bibi harusi. Hapo zamani walitumia ngamia au farasi. lakini sasa hatumia zaidi gari iliyopambwa vizuri. Baada va kushusha mavazi va bibi harusi watu huimba na kucheza na kupiga vigelegele. Aghalabu jambo hili hufanywa kabla ya wiki moja ya harusi. Kwani bwana harusi ndiye anayetaarisha mambo yote haya.

**3.2.4 Akdi**:

Siku ya akdi au nikiha (kufunga ndoa) kwa harusi za Walibya huwa ni ljumaa pili. Kama akdi itafungwa nyumbani kwa wazazi wa bibi harusi basi hufanywa asubulii baina ya saa tatu hadi saa tano. Baada ya sheikh kukamilisha zoezi la akdi hutiwa fatiha kuwaombea duwa maharusi. Kisha huandaliwa chakula. Watu wa upande wat bibi harusi luakaribisha waliohudhuria. Aghlabu huwa ni bwana harusi na jamaa zake pamoja na marafiki wa karibu kutoka pande zote mbili, chakula kinachoandaliwa huwa ni nyama iliyokaangwa mikate vinywaji. Siku hii huwa haidhuriwi na watu wengi. Katika siku hii vilevile baada ya chakula. bwana harusi anakwenda kumvesha pete bibi harusi. Aidha, bibi harusi huvaa mavazi ya kienyeji ya asili Waarabu wa Libya.

Iwapo akdi itafungwa msikitini, basi huwa ni mshuko wa Alasiri (baada ya Sala ya Alasiri). Kama kawaida huwa yuko sheikh atakave fungisha akdi, wallii wa bibi harusi (baba), bwana harusi na mashahidi. Sheihk akishamaliza zoezi la ufungisia aakdi hutiwa fatha. Baadaye watu wa Lipande wa bibi harusi hutoa tabarukil ya chakula ambacho zaidi huwa ni tende na maziwa. Kwa uifupi akdi/nikalia hufungwal kwa mujibu wa sheria ya dini va Kiisilamu.

**3.2.5 Hamam Bukhari (Mvuke):**

*Hamam Bukhari* ni ada muhimu anayofanyiwa bibi harusi wa Kilibya kama ilivyo singo va Waswahili. Siku hii bibi harusi huoshwa mwili mzima na marafiki zake. Pia hupatikana fursa ya bibi harusi kufunzwa baadhi ya mambo muhimu na ya siri katika maisha ya ndoa. Haialikiwi wala kufanyiwa sherelie kama singo ya Waswaliili. Aghlabu siku y*a "Hamam Bukhari*" huwa ni siku ya Ijumaa pili au ljumaa tatu.

**3.2.6 Siku/Yaum Khamis (kuchukua mke)**

Farha hufanywa usiku wa Alhamisi. Siku hii ndiyo siku ambayo bibi harusi anachukualiwa na bwana harusi. Siku hii kuwa bwana na bibi harusi huvaa nylo za asili ya Kilibya. Maharusi huwa wanapendeza kweli. Mavazi yao yanawakilisha utamaduni wa mavazi ya Kilbya.

Kadhalika katika siku hii hualikwa wageni mbalimbali kujua kujumuika na familia kwa uapande wa bwana harusi. Baada ya sila ya Isha wageni walialikwa huwandaliwa chakula cha kiasili ya Libya. Aghlabu huwa n*i /ja.*

**3.2.7 Yaum Dukhul (Harusi kujibu )**

Baada bwana harusi kumchukua mke wake nyumbani kwake kukutana kimwili na mkewe kwa mara ya kwanza. Huku familiya zote mbili zinasubiri kwa hamu harusi kujibu. Kila moja wanataka kujuwa kuna bibi harusi ni mtoto mdogo (bikra).

Bibi harusi akikutwa ni mtoto, bwana harusi huwajulisha marafiki zake kwa simu. Huambia. Marafiki wa bwana harusi hufahamu bwana harusi anamaanisha nini. Bila bwana harusi kuwaambia wafanye nini. Marafiki wa bwana harusi huanza kupiga rasasi juu kuashiria furaha. Baada ya hapo huingia katika magari na kwenda katika familia ya bwana na bibi harusi. wanapokuwa njiani na kukaribia kufika katika familia za maharusi hupiga honi magari kwa kupokezania, Watu wa famila zote mbili hufahamu kuwa harusi imejibu salama au kila kitu tamam.

Hapo tena kila upande wa familia hunza kusherehe keakwa kupiga vigelegele kuimba nyimbo za kuwapongeza au kuwapa hongera maharusi. Miongoni mwa nyimbo maarufu zinazoimbwa baada ya bibi harusi kuhongera ni huu hapa chini

مبروك علينا وعليكم انتم لينا واحنا ليكم

مبروك علينا وعليكم انتم لينا واحنا ليكم

Tafsiri:

*Hongereni bwana na bibi harusi sasa kila ni miliki ya mwenzake (dhamand ya mwenzake).*

Marafiki wa bwana harusi waliopeleka taarifa hizo harusi kujibu. hukaribishwa kuandaliwa chakula kidogo na vitafunio pamoja na vinywanji kama juisi soda.

**3.2.8. Al-Jihaaz, Assabaha na Asbuu (Kuwatoa Maharusi)**

hizi ni sherehe ambazo hufanyiwa bibi harusi. *Al- Jilac*e ni sherehe ambayo huwa ni siku ya Ijumaa tano. Sherehe hii inahusu watu kutoka kwa upande wa bwana harusi wanawake tu. luleta sanduku la bibi harusi. ndani ya sanduku huwa kuna : nguo, viatu, marashi na vipodozi. Siku hii bibi harusi huwa amepambwa kwa vazi la asili ya kilibya la rangi yeyote. Pia huwa amevalishwa dhahabu kochokocho. Huwa na uvimbo ambazo huinibwa na wasichana zaidi marafiki wa bibi harusi. Huwa kuna dhift pia. Siku hii ni sawa kama ile ya kumtou bibi harusi holini kwa harusi za Waswahili. Siku vil Al-Jihaaz bibi havaa nguo ya nguo ya asili ya Kilibva

sherehe hufanywa siku ya Ijumaa baada ya siku ya. Siku hii wanawake wa upande wa bibi harusi wanampa zawadi bibi harusi na kuimbu. Zawadi kama vile: pesa. zawadi, na vitu vyengine.

Asbuu *n*i siku ambayo familiya bwana harusi wanakwenda nyumbani kwa familia ya bibi harusi. Wageni kutoka upande wa bwana harusi na waalikw wengine hula chakula kama vil*e Iftar, kuskus, bazin,* na vinywaji. Siku hii bibi harusi anacheza mbele va wasichana wakiwa katika khema.

Hizi ndiyo ada kwa ujumla zinazofanywakatika harusi za Walibya. Hata hivyo, katikat mikoa au majimbo mengine kama vile Misrata. Benghazi na Tripoli hawa bila shaka wana ada tofauti kidogo na Sebha au kunyume chake. Lakini kwa ujumla wote hawa hufanya ada za harusi kulingana na siku. Yaani kuanzia siku ya Jumanne ni siku ya kulika walima, mavazi kuyapeleka kwa bibi harusi na watu kula chakula. Aidha, kila siku hadi kufikia Ijumaa kuna matendo muhimu ambayo yanafanywa.

Kadhalika, hakuna shaka watu wanaoishi vijjini na mashamba ni tofauti na wa mijini kama vile Tripoli. Sebha, Benghazi miji mengineyo. Hili ni jambo kwamba mipaka ya nchi kama vile. Tunisia, Misiri. Chad na nyenginezo pi zimeathiri mifumo na hata lugha za watu wa Libya. Ingawa wote wanasema Kiarabu lakini lazima kutakuwa na tofauti. Kwani hata watu wanaoishi katika mji mkuu wa Tripoli wameathiriwa sana na utamduni wa Ulaya katika teknolojia na mambo ya hurusi kama tunauyoona siku hadi siku.

**TOFAUTI NA KUFANANA ZA HARUSI KATI YA WAZANZIBAR NA WALIBYA**

**4.1. Utangulizi.**

Kama ilivyosemwa hapo awali kwamba kwa ujumla ada za harusi karibani jamii nyingi ulimwenguni zinafanana kihatua na kivipengele takribani lazima pawe na posa. sherehe. karamu na mengineyo kiutaratibu na kiheshima, kimila. kidesturi kami kidini ni vigumu watu wenye utamaduni wao kumili kukosa mfumo maalumu wa harusi.

Ama kwa madhumuni yetu tunataka kuangalia kwa upana kidogo tofauti na kufanana zilizopo kati ya harusi ya Zanzibar na Libya. Makala kwa kiasi fulanai imeweza kuchunguza na kubainisha hayo katika mambo yafuatayo:

**4.2. Kutafut: Mchumba**

Suala la kutafutamchumba halitofautini sana baina ya Waswahili na Walibya.

**WAZNZIBAR**

Kwa upande wa Waswhili hufanywa kwa kuzingatia haya

(1) Kwa upande wa Zanzibzri wazazi ndio humshauri watoto wa kiume waliotimu kuoa.
(2) Familia nyengine zikiona zina watoto wakike ndani wamekaa lu lawasomi al hawana jambo la msingi kwenda katika familia fulani na kushauriana wazeze watoto zao iliwaunge udugu zaidi.
(3) Mchumba anaweza kupatikana kwa kupitia mtoto wa kiume mwenyewe kusema (mimi) nnae mchumba yuko sehemu fulani au kusema mie sina mchumba mnitafutie au.
(4) Watoto wa kike na wakiume kukutana wenyewe na kupeana shauri kwamba mvulana apeleke wazazi wake kwa msichana ili wakapose.

**WALIBYA**

Ama kwa upande wa harusi za Walibya Mambo huwa kama lakini wao familia pia huuliza watoto wao wa kiume kama mchumba au. Tofauti iliyoko katika desturi ya Walibya ni dada mkubwa na mama ndio wanaokiwenda kwanzil kuuliza historia na vijana wote wawili wa kike na wakiume wa pande zote Kitu cha kuzingatia katika aina liizi za (kutafuta mchumba na kuposa katika tamaduni zao ni kwamba mara nyingi wanawake hushirikisha mwanzo kwa dhahiri na washenga huwa wao wenvenewe na kwa upanda wa Zanzibar wanaune ndio wanakuwa kipao mbele kaatika kwenda katika familia ya msichana mpaka mambo vakisha kaa sawa yote ndio wanawake wa mvulana wanaweza kwenda kwa ajili ya kuchukua vipimo vya nguo ambazo watanunua kwa ajili yake.

**4.3 Mahari Wazanzibar:**

Mambo yote haya hufanywa baada ya mahari kutoka. Lakini (pesa za mahiri) huwa ni zawadi ya mwanamke. Siku va kutoa maliri. siku hii huwa maalumu na sherehe nu kwa siku hizi bibi harusi nae hutavarishwa kupokea harusi. Watu hula na kunywa na kufurahi mahari. Kwa miaka ya nyuma ilikuwa ni shilingi 20 mpaka 2000. Siku hizi mahari yameongezeka kutokana na mambo ya kiuchumi kwa watu wa chini ni huanzia laki tano 500.000/=. Watu wa juu mahari hayo kuambiwa kutoa kwenye (milioni moja)1.000.000/ . Wengine hudai samani kama vitunda. makabati. magodoro na pesa taslimu.

Hata hivyo bado zipo familia zenye kutoza mahiri ya chini zaidi ya hayo kutegemici na uwezo wa familia hivo, au kuna makabila mengine wao ni ada yao kutoza mahari mengi. Baada ya kukamilika niambo yote yamatavansho au maandalizi ya harusi na kukatwa siku va harusi hapa tena watu hujiweka tayari kwa kufanya siku ya harusi yenyewe ambacho ndicho kilele.

**WALIBYA**

Tofauto kwa upande wa Walibva mahari hull imu zaidi. Watu wa fanila ya mke mara huitisha dhahabu na pesa taslimu. Ama kufanana ni kuwa mahari hiyo hupewa mke mwenywe kama ilivyo harusi za Wazanzibari. Pia kuna mambo mume lazima atoe kabla ya shughuli za harusi. kama *hulih war,* nyamin nakdhalika. Kwa Wazanzibuli hata mahari yanaweza kutolewa baadaye,

**4.4 Matayarisho ya Harusi.**

**WAZANZIBAR**

Kwa upande wa matayarisho ya harusi za Zanzibar baada ya posa kukabaliwa na kula kitu kuwa tayari wazazi wa wavulana (hucka) siku maalumu ya kwenda kukata siku ya harusi iwe lini na wakati gani mara nyingi harusi za Zanzibar hufanyika katika miezi ya kiislamu kama vile Mfunguo Mosi. Mfunguo Tatu. Mtunguo Nne. Mfunguo Sita na Mfunguo Tisa au Shaaban. Ni harusi chache hufanyika Ramadhani ambapo mwezi huu hawa

na gharama kidogo sana akilinganisha na miezi mengine.

Au wakati mwengine hutegemea na utokeaji wa harusi za ghafala hapa hutokea kufanyika muda muda wowote ule na pia mara nyingi harusi hufungwa siku za Ijumaa, kuendelea Jumamosi au Juma pili.

Ba*ada* va ku*k*ata siku ya h*aru*si Wazanzibari na utamaduni wao huanza heka heka za kununua vitu mbali inbali kwa familia ya msichana hununua vyomba mbali mbali vya kutumia nyumbani kama sahani sahani. vikombe, madishi. gilasi. vijito na vingi venginevyo.na kwa upande wa familia ya wavulana wao hununua nguo za kuvan biharusi alatika nyumbani kwake kama vile kanda nyingi. baibui, viatu. Vilmbaa na nguo zandani na pia vipodozi mbali inbali.

Baada ya hapo hukutana kabla ya ununuzi ili kuulizwa mama harusi kwamba anahihaji nini. Kwani kiutamaduni wanawake wa Zanzibar huwa hakosi kuweka akiba yoyote ndani ama (kanga) kwa wanaume na vyombo) kwa wanawe wanawake katika mkutano ule husema anachohitaji yeve ni nini zaidi na baadae hupigwa thamani ya pesa na kila mmoja hutoa kiwango chake alichopangiwa na mambo mengine walivyo kubaliana Na pia mwisho hupanga kikao au mkutano wa mwisho na kutathmini kilichopatikana na kilichopungua na kufanya majumuisho na kuziba mpengo madogo madogo ya maandalizi ya shughuli.

**WALIBYA**

Walibya huwa na matayarisho au maandalizi ya kabla ya harusi na wakati wa harusi na baada ya harusi.ya harusi walibya nao pia hujiandaa kwa harusi kwani baada ya kama tulivyoona baadae ya koo mbili kukutana na baadae familia ya msichana kukaa pamoja na kukata mahari.hapo tena kwa hatua za awali bwana harusi na familia yake wao ndio hasa wafanyaji shughuli ukilingalinisha. Ama harusi za Zanaibar pande zote mbili kila mmoja zinachangia Tofauti kubwa iliyopo katika matavarisho ya harusi baina ya Walibya na Wzanzibar ni kuwa siku za harusi kwa upande Wazanzibari ni chache lakini idadi ya siku y:1 harusi za Walibya ni nyingi takriban wiki nzima. Harusi huanzia siku ya Jumanne hadi Ijumaa kama tulivyoona. Na kila siku huwa na shughuli yake.

Kwa hivyo hapa katika maandalizi ya harusi Zanzibar hujikata zaidi katikat kukusanya mahitaji mbali mbali kuanzia Vyombo, nguo(mavazi).ngoma shereha. dhifa na karamu mpaka chakula cha biharusi lakini Libya wao ni bwana harusi kupclcka waliima vaani chakula kitakachotumika nyumbani kwa mwanamke wakati wa harusi

**4.5 Singo au *Yaum Bukhar:i***

**WAZANZIBAR**

Tofauti iliyoko ni kuwa katika Zanzibar bibi harusi *anaanza* kuwekw*a ndani 1* kutayarishwa na kupewa mafunzo mbali mbali ya unyago pamoja na kusingwa. Watu hualikwa hasa wake waliolewa. Huimba nyimbo mbalimbali za kumfunza mke kukaa vizuri katika nyumba yake na mumewe.

**WALIBYA**

Wao hawaaliki na hiyo sio sherehe rasmi. Na wanamsinga bibi harusi na marafiki zake wasiozidi wawili

**4.6 Hinna**

**WAZANZIBARI NA WALIBYA**

Katika upakaji wa hina katika harusi za Zanzibar hupakwa kabla ya harusi lakini hupangwa siku maalumu ya hina ila sio kama Libya kama lazima iwa Jumatano il kama ilivyo ada yao. Zanzibar lutegemea siku ya shughuli ilivyopangwa na huchaguliwa siku moja watu wakatanya siku ya hini na katika siku hii aghlabu bi harusi anakuwa tavari ameshachora hina vizuri na watu wengine wanachukua ima ujiti au koni na kumpaka kwa kufuatanisha nakshi va mwanzo ikiwa imefanyiwa STEI .

Ila wengine hawafanyi siku ya hinna kama ni sherehe maaluma hasa kutokana na masuala ya kiuchumi nauwezo mtu ima anakuja nyumbani au bi harusi anakwenda kupakwa hina na kurudi tu pasi na kusubiri siku ya harusi ifike.

**4.7 Mavazi ya Akdi**

**WAZANZIBARI NA WALIBYA**

Kawaida kwa Wazanzibar nguo za bi harusi huwa mbili yaani siku ya akdi yaani siku ya kufunga ndoa huwa ni nguo ringi va kijani ni siku ya bi harusi akichukuliwa huwa ni nguo rangi nyeupe.

Bwana harusi mara nyingi huwa hana gharama sana. Nguo zake huwa ni al buslili na kanzu nayo hii havaliwa kwa kilemba cha kijani au kama joho na kilemba cheusi al chekundi au wengine huvaa kanzu koti na kofia na hii ndio asili ya Mswahili Wit Zanzibar. Kama tulivyosema katika Zanizibar watu hufanya harusi kwa taratibu nyingi zenye tamaduni tofauti.

Na wale ambao watapenda kwenda holini basi mara nyingi huvaa suti lakini wengine huenda hivyo na majoho, kanzu, makoti yao katika holi.

Kwa upande harusi za Walibya takribani siku ya akdi huwa na nguo maalumu. Nguo hizi huo ni za asili ya Kilibya. Bibi hurusi huvalishwa pamoja na mapamboa ya dhahabu. Huku bwana harusi huva kawaida kanzu na kofia. Kwa harusi za Walibya siku ya akdi haishangiriwi sana kama harusi za Wasawahili. Walibya hushangiria zaidi siku ya *farha-* siku ya kuchukua mke au 1 *kramtis.*

**4.8 Siku ya HIlarusi au kilele cha Ilarusi:**

**WAZANZIBRA**

Kwa upande wa Zanzibar siku ya harusi huanza na kitendo cha kufunga ndoa ya. Akdi na kwa kweli siku hii ndio siku adhimu na furaha kede kede kwa familia, ndugu na majirani.

Kikawaida katika siku hii watu huvaa vizuri wanawake na wanaume. Huwa na hoi hoi watu wote hukaa na wasiwasi mpaka ndoa ilanwe. Yaani bibi harusi awe mke halali kwa bwana harusi na ile kauli ya uchumba inalizike.

Akdi mara nyingi kwa kizamani au mpaka ndoa kutungwa baada ya sala ya Adhuhuri au Alaasiri. au Magharibi au baada ya sulat Ishaa. Akdi wakati huwa alfajiri au asubuhi ya mapema mara nyingi ljumaa au siku yeyote.

Kama Akdi imefunywa asubuhi au Alifajiri mara nyingi bibi harusi huachwa na kuja kuchukuliwa jioni au usiku. Lakini kana ni jioni basi mara nyingi bi harusi huchukuliwa pale pale na kupeleka kwa mumewe lakini kabla ya kuondoka tayari huwa ameshashikwa kichwa na kusomewa dua na mumewe na bwana liarusi na sheikh au kadhi waliokuja nac.

Wauine waliokuja kuowa tena huondoka na kurudi makwao na huku wakiimba nyimbo au tumbuizo mbali mbali za kuonesha furaha juu ya harusi waliohudhuria tumbuizo hizo ni kama vile.

Tunaomti tunao ,twende nao pole pole. Tunkaupasue mbao, mashine hadi malele Tukaupasue mbao, mashine hadi malele.

Tumbuizo hizo mara nyingi huimbwa na wanawake wakiwa wamevalia nguo vizuri na kujipamba.

**WALIBY*A***

Kama tulivyosema hapo awali katika Libya mambo yote ya harusi yanaendana na siku maalumu. Kwa hivyo siku ya ndoa hasa huanzwa Jumatatu au wengine hufanya Jumanne hapa baba wa bibi harusi pamoja na kadhi au sheikh na bwana harusi : watu wengine takariban

ishirini (20) Wanakala katika hema au msikitini au palali popote walipopanga na kutanva ndoa yaani "Akdi" na baadae bwana harusi anakwenda kumvisha pete bwana harusi na hapa luvaa mavazi ya kienyeji ya asili Waarabu wa Libya.

Tofauti nyingine ni kuwa bwana harusi anapeleka nguo kwa bibi harusi ili kutayarisha nguo ya kuvaa siku ya akdi. Wazanzibari hawafanyi hivyo nguo ya bi harusi yalok! upande wao. Baada ya hapo luula na kunywa na kufurahi na kucheza na kupiga vigelegele kwa furaha na bibi harusi bado hubakia nyumbani kwao na kuendelea an mambo mengine kwani harusi ya Libya inamlolongo wamambo mengi sana.

Kwa hivyo siku ya kufanya ndoa huwa si mambo mengi kama ilivyo hapa Zanzibar kwani baada ya hapo watu hujiandaa na sherehe za liarusi kana ilivyoida.

Kama tujuavyo Walibya wengi ni Waislamu kwa hivyo mambo mengine yanafanana na harusi ya hapa Zanzibar. Kwa sababu wanendesha mambo yote kwa mujibu wa sharia ya Kiislamu.

**4.9 Sherehe Baada va Akdi**

**WAZANZIBAR**

Katika Zanzibar sherehe za harusi mara nyingi hutegemea na uweza wa familia kwa ujumla kwani mara nyingi sherehe za harusi huambatana na ngoma au tumbuizo au kaswida pamoja na maulidi.

Hii ni kutokana na watu kiuwezo pamoja na maadili yao. Watu wengi wenye uwezo wengine husoma kwanza maulidi siku ya akdi na sherehe kabisa, lakini pia hupanga siku nyengine mbali katika kumbi kubwa maalumu kwa ajli ya kucheza na ngoma za taarabu au rusha roho. Mwisho hula na kunywa na kupeana zawadi kwa watu mbali mbali walioalikwa.

Wengine huchanganya sherehe ya harusi ya *"bug parü*" pamoja "*kirchen porn* vitu hivi hufanywa kabla ya harusi ili kuchangia sanduka au mbajo na wengine huchangia vyomba vya jikoni na bibi harusi husimama pale na kupokea zawadi mbali mbali kutoka kwa ndugu, jamaa na marafiki.

Hivyo basi .bibi harusi na mumewe tena baada ya siku ya pili au ya tatu hupelekwa *saloon*" na kutengenezwa nywele na mapambo mengine ya mwili na hina na hapa ndopo pale anapopandishwa katika "*sage*",

Bibi harusi huingia ukumbini akiwa amefuatana na washaika veli. Yaani watoto kuanzia wawili na kuendelea wakiwa wamevalia nguo zilizofanana na bibi harusi kwil moja.

Kama ni wanawake, na wanaume nao huvaa suti kama ya bwana harusi wako. *Bridemaid*s huwa wameshika vikapu vya harusi vyenye mata yanayonukia kama asumimini au mawardi ya rangi ya pinki. Huyarusha rusha usoni na pembeni atakapopita bibi harusi na bwana harusi.

Baada ya hapo mmoja kati ya wale washika veli Yaani *bride acties* liuwa na kisusu ambacho ndani yake huwa na pete ya dhahabu na wenye uwezo wao huwa ni pele vil almasi. Pete hizi huwa mbili moja ni ya bwana harusi na yeye ndio wa mwanzo kuchukua mwanzo na kumvesha mkewe.

Na pia kwa upanda wa upande wapili bwana harusi huveshwa pete na mkewe na hapo teno huleta keki. Baadaye watu hulishana keki vaani huanza bibi harusi kumlisha mumewe keki na bwana harusi nave hukata kipande cha keki na kumlists: mkewe. Kitendo hicho kikimalizoa tena keki hukatwa na kulishana watu wote wa familia, ndugu, wapenzi na marafiki.

Kikimalizika kidogo kutendo hicho watu hupiga picha. Picha za awaida na ya video. Wakati mwengine huweka muziki au kuimba kasida za kumsifu mke na munc. Utakuta kuna mchangaiko ya Ya kizungu na Kiswahili kwani katika kipengele liiki cha sherehe na harusi kwa ujumla mambo yote haya huchanganyika na lantaduni tfauti tafauti utakuta za Kizungu. Kiarabu. Kihindu na Kiswahili.

Mara nyingi shughuli huendelea mpaka saa sita usiku, ikiwa harusi imeanza saa mbili mwisho wa hapo maharusi wote wawili pamoja na wapambe wao hurudi nyumbani kwa ajili ya kupumzika na kuendelea na fungate yao.

**WALIBYA**

Kama kawaida na hili huanza kwa kuzingatia siku maalumu kwani baada ya ndoa kufungwa kinachofuatiwa ni sherehe. Sherehe zao ni tofauti kidogo na Zanzaibar. Kwani baadhi ya mambo sisi watu wa Libya hufanya baada ya ndoa lakini Zanzibar wao huyafanya kabla ya ndoa kufanvika.

Kwa kawaida katika Libya, baada ya siku ya Jumatatu au Jumanne kufanya akdi uatwa ni harusi yaani shere ya harusi. na wao kwa kawaida Jumanne bibi harusi sherehe yake huanza na hapa mara nyingi bi harusi huvaa nguo nyeupe na kupambwa vizuri yaani huvaa "r*eli*" kama katika harusi ya wa zungu. Vilc hili hutiwa pamoja na mapambo ya fedha na dhahabu nyeupe iliyopambwa kwa fedha. Bwana harusi naye huvalia vizuri kwa suti na kupelekwa holini na watu wote kufurahi mat kucheza vizuri na kula chakula pamoja na mumewe na watu wote waleo hudhuria katika sherehe ile.na baada ya kurudi katika sherehe ile usiku wa Jumanne kuanikia Jumatano hapa hufanywa siku va*hina y*aani yaumul-bina. Hina hutiwa mikononi tu niwa bi harusi katika *yaumul-hia.* Kila mtu huenda na kumpaka bib harusi hina hivyo katika viganja vyake viwili vya mikono kwa kufuatisha mauwa ya initindo ya Kilibyu. Kwa ufupi hina hukesha usika wa kucha na watu labda hupumzika kidogo.

Sherehe hii inafanywa baada ya ndoa kufungwa yaani akdi wakati huu waakadi bibi harusi wanavaa mavazi ya Kiarabu yenye asili ya Libya na mapambo *ya Li*bya.

Baada ya hapo sherehe ya harusi huendelea mpaka katika siku Jumatano ambayo siku hii ndio siku ambayo bibi harusi huvaa dhabu na nguo rangi ya dhahabu na mapambo va dhahabu ya harusi.na hapa kwanza huwa wevaa nguo ya nyumbani kwao, lakini waume wanapokuja huivua na kumvalisha nguo ya mume pamoja na kula chakult kitamu sana na nyama na vinywaji. soda, juisi nakadhalika.

Na baada ya kushusha mavazi kaktika siku hii watu au wazazi wa bwana harusi huimba na kufurahi vizuri na kuchangamkana na kusaliana pamoja na baada kurudi nyumbani kwao, lakini kwa kawaida ya Libya biharusi hawa hachukuliwi siku ile kwani huachwa kwao mpaka siku maaluma na shere zilamaliza nduo aenda kwani Sherehe huendelea tena kwa siku ya Ahmisi subuhi na hii huitwa siku ya *"mirnalr".* Yauma-mirwah ni siku kuondoa bibi harusi kwenda kwake na bwana harusi au kwenda ukweni kwake.

Siku hii huwa na mambo mengi sana katika kusherekea kwake. Asbuhi ya siku hii ya Alhamisi bibi akiwa kwao husuka nywele ndogo ndogo au nyembamba kiasi cha nywele silini. Nywele hizi husukwa na mikia yake huanguka mpaka chini na hapa bibi harusi huvaa nguo rangi yeyote.

Baada ya kufanya haya. watu hupiga ngoma na kucheza na wengine hula, hungwa chakula na vinywaji vizuri visivyo na uleui.

Punde bwana harusi na familia yake huja na magari yao. Gari la bwana harusi hupambwa vizuri kama ada. Tlupambwa kwa riboni na mabofu au baluni, na hapa wakifika huko katika familia ya bwana harusi mara nyingi huenda wanawake tu. Na wanaume walioko huko huandaliwa chakula msikitini na wanawake hukaa nyumbani na kula chakula na bibi harusi.

Na baada ya hapo hufuatia siku ya ljumaa. Familia ya bibi harusi wanakwenda nyumbani kwa bibi harusi na bwana harusi kwa upanda wa wakwe zote na pia wanasaidia kidogo familia ya bwana harusi kutayarisha chai na chakula cha asubuhi na kutayarisha chakula cha jioni au mchana. Baadaye bibi harusi anapambwa vizuri na kuvau kanzu nyeupe pamoja na mapambo meupe yaani fedha Lupu. Bwana harusi huvaa kanza ya kienyeji baadaye wanapelekwa katika sehemu au ukumbi wanakaa na kupokea zawadi nyingi sana kutoka kwa watu mbali mbali.

Baadaye bibi harusi anapambwa tena vizuri kwa mavazi meupe na mapambo kama zawadi mbali mbali bibi harusi anatoka anakwenda kahamia nyumbani kwake.

**4.10 Harusi Kujibu**

**WAZANZIBAR na WALIBYA**

Familia ya maharusi hujuwa kama harusi imejibu kuptia kwa makungwi au bwana harusi mwenyewe kuwaeleza. Au kwa zanzi wanawake hujipaka mashinzi usoni. Kwa upande wa Walibya marafiki ndio hupiga bunduki juu wana imba na kwenda na magari huku wakipiga mahono. Matendo haya kila mtu anafahamu kuwa harusi imejibu salama.

**HITIMISHO**

Makala hii ilikuwa na sura tano (5). Sura ya kwanza tulieleza msingi wa makala huu. Tulieleza mambo kama vile: usuli wa mada, tatizo la utaliti, madhuniuni ya Makala, maswali ya makala, umuhimu wa makala, eneo na upeo wa makala, ukusanyaji wa data na kutoa maana ya istilahi zilizotumika.

Sura ya pili tulielezea taratibu ya harusi za Wazanzibar na ada zake. Aidha, Sura ya latu tuliangalia tena taratibu za harusi za Walibya. Uchunguzi wa kubainisha tofauti na kufanana kati ya harusi za Wazanzibar na Walibya zilielezwa katika sura ya nne. Masuala kuhusu muhtasari na hitimsho valielezwa katika sura la tano.

Kwa kuhitimisha tofauti hizi harusi na ada zake kati ya Walibya na Wazanzibar tunasema kwamba kuna tofauti nyingi katika vipengele mbali mbali katika harusi.za jamii hizi mbili. Hata hivyo kuna mambo kadhaa valiyojitokeza ambayo wakati wa harusi au baada ya harusi kama vile katika Zanzibar bi harusi laci kwa wala kwa wakwe mpaka aitwe ugeni au walikwe kushinda na kukaribishwa lakini katika Libya mambo haya ni tofauti.

Hali kadhalika suala la Zanzibar kuwa na tamaduni tofauti ambazo kila kipengele huingia na kuchangia, kwani hakuna kipengele katika harusi ya Zanzibar isiyoingiliwa na kipengele kimoja wapo cha kigeni kama vile ada Kiarabu. Kingazija. Kizungu pamoja na zile za asili ya watu wa Zanzibar.

Kwa ufupi kuna tofauti kubwa katika kipengele cha matayarisho au maandalizi ya shughuli kati ya Zanzibar na Libya kwa upande wa harusi. Kama tulivyosema maandalizi ya shughuli.

Kwanza ni hatua za awali wakati wa posa na kutafuta mchumba mipaka kusimama posa na kutoa mahari. Pili watu kukubaliana na kuandaa harusi kwa kutafuta mahitaji mbali mbali ya shughuli nzima. Baadhi ya vipengele hivyo ni pamoja na:

(a) Kutafuta vyombo kwa watu wa bi harusi.
(b) Kutafuta sanduku kwa watu wa bwana harusi.
(c) Kualika watu harusi au jaliko kwa zamani.
(d) kupanga mipango ya harusi kwa familia zote mbili
(e) Kuhusu karainu, dhifa na chakula cha bi harusi.
(f) kupanga pahali pa kufanyia harusi pamoja na harusi itakuwa siku ngapi kwa mujibu wa hali za watu kiuchumi na kimaadili.
(g) Kutafuta nguo za kuvaa bibi harusi na bwana harusi kwa kila mtu na familia yake. Bi harusi peke yao na bwana harusi peke yao.
Kumtayarisha bibi harusi kwa mambo ya usafi na mapambo kama hina ina mengine.

Yote haya hufanywa kabla ya ndoa kufanywa kidesturi na kiutamaduni.

Matayarisho ya harusi kwa upande wa Libya.

(a) Mchumba mara nyingi huanza kutafutiwa na dada mkubwa na mama wa bwana harusi.
(b) Bwana harusi na familia yake hutafuta nguo za bibi harusi na mapambo ya dhahabu. fedha na mengine.
(c) Bwana harusi na familia yake kupeleka chakula yaani waliima kwa familia ya bib harusi.
(d) Kufanya karamu kabla ya wiki moja ya harusi kwa upanda wa bwana harusi na baadae kutika kwenda kupelcka mavazi na chakula kwa biharusi .
(e) Yote haya hundumu kwa siku maalumu kuanzia Jumanne mpaka Ijumaa,

Hivyo basi kuwa ufupi tunaweza kusema kuna mambo mengi yanayofanywa lakini hatuwezi kuelezea kila kitu kutokana na haja iliyopo. lakini kadiri tutakavyo endelea kadh yahusuyo harusi kwa jamii zetu mbili hizi zenye tamaduni tofauti pamoja na mila na silka zetu za Kilibya na Zanzibar

**Marejeo**

Fary. M.S.A (1956) A*da za Hurusi katika Unguja.* East African Literature Bureau. Nairobi.

Mohamed s.m (1*972) Kiu* Dar-es-Salaam. Educationl Books. Publishers Ltd.

Kanduru A.S (1988) *Harusi w Gliarca.* Dar-es-Salaam. Educational Book Publisher.

BAKIZA (2010) *Kamusi vu KisHalili Fasaha* Baraza la Kiswahili Zanzibar, Offord University Press.